`HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31/03/2019

Mh. Mwenyekiti,
Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango
Hiki ni kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha kujadili taarifa mbalimbali za Fedha, Uongozi na Mipango. Kikao hiki kinafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya 1982 ikisomwa pamoja na marekebisho yake na Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya 2009 agizo namba 21.Kwa msingi huo ni jukumu la kila mjumbe kupitia taarifa hii na kuchangia maoni ambayo yataisaidia Halmashauri kufikia lengo kuu la kutoa Huduma nzuri na endelevu zenye kuleta Maendeleo katika Wilaya yetu ya Mufindi.

1) **Mapitio ya Bajeti 2018/19**

A) Mapato
Mh. Mwenyekiti,
Katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilipitisha bajeti ya kukusanya na kupokea jumla ya **Tshs.56,359,048,777.00** Makusanyo haya yamegawanyika kama ifuatavyo;

Na.	Maelezo	Kiasi
1.	Mapato ya ndani	4,162,017,000.00
2.	Ruzuku Mishahara	35,229,626,720.00
3.	Ruzuku matumizi ya kawaida	1,312,132,000.00
4.	Ruzuku ya miradi ya maendeleo na Wadau wengineo	10,856,660,057.00
5	Nguvu za Wananchi	4,798,613,000.00
JUMLA		**56,359,048,777.00**

Aidha kwa mwaka wa fedha 2018/19, Halmashauri imeanza na bakaa ya**Tshs.1,164,911,096.50** Fedha hizi zimegawanyika kama ifuatavyo;

Jina la akaunti	Namba ya akaunti	Kiasi
Matumizi ya kawaida	9921210901	12,454,597.38
Miradi ya Maendeleo	9921210301	217,787,291.25
Maji	9921210701	38,715,509.76

Mapato ya ndani	60210001172	381,520,394.05
Akaunti ya Mishahara	9921210801	2,563,371.32
Elimu	9921210501	78,934,966.37
Afya	9921210601	432,934,966.37
Jumla		**1,164,911,096.50**

Mh. Mwenyekiti

Ukijumlisha fedha ya bakaa, makisio yaliyokuwa yameidhinishwa, bajeti ya Halmashauri kwa Mwaka 2018/2019 inakuwa na jumla ya **Tshs.57,523,959,873.50** kwa mchanganuo ufuatao;

Chanzo cha Mapato	**Kiasi**
Mapato ya ndani	4,608,093,466.37
Ruzuku ya Mishahara	35,229,626,720.00
Matumizi mengineyo	1,436,134,563.67
Nguvu za Wananchi	4,798,613,000.00
Miradi ya Maendeleo	11,451,492,123.46
Jumla	**57,523,959,873.50**

B) Matumizi

Mh. Mwenyekiti

Katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Halmashauri ya wilaya ya Mufindi inategemea kutumia jumla ya **Tshs.57,523,959,873.50** Matumizi hayo yamegawanyika kama ifuatavyo;

Chanzo cha Matumizi	**Kiasi**
Mishahara	35,229,626,720.00
Matumizi ya Kawaida	3,447,988,563.67
Miradi ya maendeleo	18,846,344,589.83
Jumla	**57,523,959,873.50**

2) Hali Halisi

A) Mapato

Mh. Mwenyekiti,

Katika kipindi cha Julai 2018 hadi March 2019, Halmashauri ilikusanya na kupokea jumla ya **Tshs.27,459,845,059.25** Kati ya Mapato haya **Tshs. 3,057,338,152.56** ni mapato yaliyotokana na vyanzo vya ndani, **Tshs.18,597,553,824.83** ni ruzuku ya Mishahara, **Tshs.4,855,241,252.50** ni ruzuku ya Miradi ya maendeleo na **Tshs.949,711,829.36** niruzuku ya Matumizi ya kawaida.

Mlinganisho wa Mapato halisi ya **Tshs 27,459,845,059.25** kwa kipindi cha Juali 2018 hadi March 2019 na makisio yaliyoingizwa kwenye Mfumo ya **Tshs. 55,716,176,287.72** ya mwaka 2018/19 unaonesha kuwa Halmashauri imekusanya na kupokea asilimia **49.29** ya lengo la mwaka wa fedha wa 2018/2019. Aidha mlinganisho wa mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani yaliyokusanywa kwa kipindi cha Julai 2018 hadi March 2019 ya **Tshs. 3,057,338,152.56** na Makisio ya mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani ya **Tshs.4,162,017,000.00** kwa kipindi hicho, yanaonesha kuwa Halmashauri imekusanya asilimia **73.46** ya lengo la mwaka .

Mh Mwenyekiti,

Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha Julai 2018- March 2019 unaonesha kuwa hali ya ukusanyaji wa mapato sio nzuri sana.
Hali hii inasababishwa na

- Kukosekana kwa watendaji kwa baadhi ya vijiji na watendaji wengine kutokuwa waaminifu kwa kutumia fedha za mapato wanayokusanya na hivyo kufanya mashine za kukusanyia mapato kubakia ofisini.
- Wafanyabiashara kukwepa kulipa ushuru wa mazao ya misitu na mazao mengineyo
- Kutokusanya leseni za biashara,leseni za vileo, ushuru wa nyumba za kulala wageni kama ilivyo kwenye bajeti kutokana na uhaba wa watumishi katika kitengo cha Biashara hata hivyo tumeanza kuongeza watumishi kwenye kitengo cha Biashara kwa kumpeleka mtumishi mmoja.
- Kuchelewa kuunganishwa na mfumo wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi unaowezesha kufanya miamala ya mauzo ya viwanja vilivyopo Mji mdogo wa Igowole
- Kuwepo kwa Mvua nyingi kipindi cha March na hivyo kushuka kwa idadi ya mbao zilizosafirishwa
- Watendaji wa Kwenye vizuia kutofanya kazi kwa weledi na hivyo kufanya wafanyabiashara wa mbao kutolipa ushuru stahiki
- Mwamko mdogo wa wananchi katika kuchangia mfuko wa Afya (CHF)

Ili kukabiliana na hali hii Halmashauri imejipanga kufanya yafuatayo

- Kufanya doria kila siku ili kubaini wafanyabiashara wanaotorosha mazao ya misitu na mazao ya mengineyo bila kulipia.
- Kuanzisha Vizuia kadiri itakavyoonekana inafaa
- Kuendelea kufanya ufuatiliaji wa ununuzi wa gari la mapato ili kuongeza vyenzo za kufanyia kazi.
- Kuanzisha/kutenga maeneo ambayo yatatumika kama Soko la kuuzia mazao ya misitu ili kupunguza gharama za ufuatiliaji. Kwa kuanzia Halmashauri imeanza na Soko la mtili
- Kuwachukulia hatua za kisheria watendaji watakaotumia fedha za makusanyo

- Kila idara kusimamia chanzo cha mapato ili kuhakikisha kinakusanywa kulingana na makisio iliyojiwekea na kukitolea taarifa katika vikao vya Kamati ya fedha ,Uongozi na Mipango
- Kusimamia matumizi ya Mfumo wa Ki Electronic wa ukusanyaji wa mapato kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara.
- Kuendelea kuongeza mashine (POS) za kukusanyia mapato ili maeneo ambayo hayajapata Machine yapate
- Kuendelea kuwatambua Wafanyabiashara wanaofanya biashara katika Eneo la mamlaka ya Halmashauri ya wilaya ya Mufindi ili waweze kulipa kodi na Leseni za Biashara na kuendelea kutumia kikosi kazi cha kukusanya leseni za biashara ili kufikia malengo.
- Wakuu wa idara na wasaidizi wao kupangiwe zamu ya kuwepo katika maeneo ya vizuia kila siku ili kuongeza uwajibikaji katika vizuia. Aidha, kuwapunguza watumishi na vibarua waliopo katika vizuia ili kupunguza gharama za uendeshaji.
- Kuendelea na uhamasishaji kwa Wananchi kuhusu uuzwaji wa viwanja vya Igowole baada ya kukamilika uunganishwaji wa Mfumo wa kielektroniki wa Wizara ya Ardhi na kuwakumbusha watumishi waliokopeshwa viwanja kulipa kwa wakati uliokubalika
- Kuendelea kuhamasisha Jamii kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii

B) Matumizi

Mh. Mwenyekiti,

Matumizi hutegemea mapato yanayokusanywa. Kwa kipindi cha kuishia 31, March 2019, Halmashauri imetumia kiasi cha Tshs. 24,838,168,669.65 Matumizi hayo yamegawanyika kama ifuatavyo,

Chanzo cha Matumizi	**Kiasi**
Mishahara	18,564,792,840
Matumizi Mengineyo	2,288,019,393.65
Miradi ya Maendeleo	3,096,750,512.48
Jumla	**24,838,168,669.65**

3) Taarifa Nyinginezo

a) Usuluhisho wa Benki

Mh. Mwenyekiti,

Kutokana na kufunguliwa kwa akaunti za Halmashauri Benki kuu ya Tanzania (BOT) , Halmashauri zilielekezwa kufunga baadhi ya Akaunti zilizoko NMB baada ya miezi sita kupita tokea kufunguliwa kwa akaunti zilizoko BOT. Akaunti ambazo zimebakia NMB ni Akaunti ya Mapato ya Ndani na akaunti ya Amana. Usuluhisho kwa akaunti hizi za NMB

haujafanyika kutokana na mapato mengi kuingia mara mbili na hivyo kuhitaji kufuta baadhi ya maingizo yasiyo sahihi. Zoezi la kufuta maingizo yasoyo sahihi linaendelea kwa ushirikiano na TAMISEMI. Kwa akaunti zilizoko BOT usuluhisho wa vitabu haujafanyika kutokana na kutopatikana kwa "Cash book" za Treasury single account. Hata hivyo mafunzo ya ufanyaji wa usuluhishi wa vitabu hivi yamefanyika mwezi January 2019 na ofisi inasubiri maelekezo mengine juu ya upatikanaji wa Cash book hizo

b) Akaunti ya Amana

Akaunti ya Amana huweka amana mbalimbali. Wakati tunaanza mwaka huu wa fedha (1/7/2018) mfuko huu ulianza na salio anzia la **Tshs.282,859,579.41** Mapato kwa mwezi Julai - March 2019 yalikuwa **Tshs.678,700,544.19** na hivyo kuifanya Akaunti hii kuwa na jumla ya **Tshs.961,560,123.60** ilipofika tarehe 31/03/2019. Aidha Matumizi kwa Mwezi Julai – March 2019 ni Kiasi cha **Tshs.353,805,793.63** na hivyo kufanya Akaunti hii kuwa na bakaa ya **Tshs.607,754,329.97**

c) Madeni

Mh. Mwenyekiti,

Halmashauri imefanya uhakiki wa madeni na kwamba kuanzia 1 Julai 2018 Halmashauri ilikuwa na deni la Tshs **311,190,046.70** ,ambapo hadi kufikia March 2019 jumla ya deni la Tshs **77,443,995.50** lilikuwa limelipwa na kusalia kiasi cha Tshs **233,746,051.20**

Mh. Mwenyekiti,

Pamoja na Taarifa hii nimefungasha Jedwali Mbalimbali zinazoonesha mwenendo wa mapato na matumizi katika kipindi kinachoishia March 2019.

Mh. Mwenyekiti,

Naomba Kuwasilisha.

Felis B.Mhando
KNY: MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
MUFINDI